

SEKTA YA ELIMU:

Hali halisi ya Idara ya Elimu Katika kipindi cha Miaka 50 tangu Uhuru ni kama ifuatavyo;-

1.SERA NA SHERIA ZILIZOKUWEPO NA ZINAZOONGOZA TAASISI.

SERA:

- (i) Mwaka 1962 - Sera ya kuondoa ubaguzi katika Elimu Kabla ya hapo kulikuwa na Shule tofauti za wazungu, waasia, na waafrika.
- (ii) Mwaka 1964 – Sera ya kujitosheleza katika wataalamu wake yenyewe ifikapo mwaka 1980.
- (iii) Mwaka 1967 – Sera ya Elimu ya Kujitegemea.
- (iv) Mwaka 1970 – Sera ya kufuta ujinga wa kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu.
- (v) Mwaka 1974 – Sera ya Elimu kwa Watoto wote (UPE)
- (vi) Mwaka 1990 – Mkutano wa Dunia kuhusu Elimu na Haki za Watoto (EFA) – Mkutano zililenga kwenye Elimu ya Watu Wazima na Elimu kwa watoto wote wenye umri wa kwenda shule.
- (vii) Sera ya 1995 - Elimu ya Mafunzo inayoelezea uendeshaji wa Shule za Msingi na Sekondari.
- (viii) Sera ya 1995 – Sera ya Elimu na Mafunzo inayowataka Wazazi kuchangia gharama za Elimu ya watoto wao.

SHERIA:

1978 – Namba 25 – Mahudhurio ya lazima kwa Mwanafunzi.

1995 – Uendeshaji wa Idara ya Ukaguzi.

3. MAFANIKIO YALIYOPATIKANA / FURSA ZILIZOPO:

- Ongezeko la Shule za Msingi na Sekondari.
- Kupanda kwa Uandikishaji katika Shule za Msingi.
- Uwepo wa Madarasa ya Elimu ya Awali katika shule zote za Msingi.
- Uwepo wa vituo vya Chekechea.
- Utolewaji wa fedha za Uendeshaji Shule za Msingi na Sekondari (MMEM & MMES)

A. ELIMU YA MSINGI

NA		MWAKA 1961	MWAKA 2011
1	Shule za Msingi	22	321
2	Madarasa	110	1991
3	Nyumba za Walimu	66	1080
4	Idadi ya Walimu	110	2021
5	Idadi ya Wanafunzi	4000	100,133

B. SEKONDARI

NA		MWAKA 1961	MWAKA 2011
1	Idadi ya Sekondari	1 ya Mission	61

2	Idadi ya Wanafunzi	35	16,672
3	Majengo ya Utawala	1	36
4	Idadi ya Madarasa	1	599
5	Hostel	0	6
6	Nyumba za Walimu	2	153
7	Maktaba	0	9
8	Bwalo la Chakula	0	4
9	Idadi ya Walimu	4	540

C. VYUO

NA		MWAKA 1961	MWAKA 2011
1	Chuo cha Ualimu	0	1
2	FDC	0	1

MABADILIKO KIUTAWALA

- Kuwepo kwa Maafisa Elimu Wilaya wawili katika Idara ya Elimu mwaka 2008 ambao ni Afisa Elimu Msingi na Afisa elimu Sekondari.
- Elimu ya Sekondari kuhamishiwa Serikali za Mitaa mwaka 2008.

4.0 CHANGAMOTO

1. Kushindwa kueleweka kwa Sera ya Elimu ya Kujitegemea (Education for Self reliance)
2. Kubadilika badilika kwa Vitabu Elimu. Mtazamo hasi kuhusu Elimu ya Watu Wazima.

3. Upungufu wa vifaa vya kufundishia na kujifunzia.
4. Upungufu wa Maktaba katika Shule za Msingi, Sekondari, Kata na Wilaya.
5. Uchakavu wa majengo ya Shule.
6. Upungufu wa vituo vya Ufundi Stadi usioendana na wingi wa wanafunzi wanaohitimu Elimu ya Msingi na Sekondari na kukosa ajira.
7. Lugha ya kufundishia.
 - (i) Uwepo wa Walimu wenye Taaluma ya kutosha.
 - (ii) Upungufu wa Walimu
8. Upungufu wa Samani.
9. Ukosefu wa chakula shuleni
10. Utoro.

5.0 MATARAJIO YA TAASISI MIAKA 50 IJAYO

- (i) Kujenga Madarasa ya Elimu ya Awali katika Shule zote za Msingi.
- (ii) Kujenga Maktaba za Shule na Kata katika Kata zote.
- (iii) Kuboresha miundo mbinu yote ya Shule za Msingi na Sekondari.
- (iv) Kuondoa kabisa tatizo la kutojua kusoma, kuandika na kuhesabu katika Wilaya kwa wanafunzi na Watu Wazima.
- (v) Kuanzisha vituo vya Elimu ya Sekondari kwa kushirikiana Taasisi ya Elimu ya Watu Wazima katika Kata zote.

Kujenga Maabara kwa shule zote za Sekondari.